JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

-------------

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. PHILIP I. MPANGO (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2016/17 NA MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2016/17

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

**FEBRUARI, 2016**

**MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. PHILIP I. MPANGO (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2016/17 NA MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2016/17**

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kuishauri Serikali kuhusu **Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17** na **Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2016/17**.

2. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kwa ushirikiano wao. Maelekezo na ushauri mzuri waliotupatia wakati wa kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/17 na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2016/17, umetusaidia katika kuandaa hotuba hii na kuboresha hatua za maandalizi ya Mpango wenyewe. Kipekee nimshukuru Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb), na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Servacius Beda Likwelile kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu pamoja na maandalizi ya hotuba na kuandaa vitabu hivi.

## MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 2016/17



3. **Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo

wa Taifa wa Mwaka 2016/17 ninayowasilisha leo katika Bunge lako Tukufu yatatumika kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17. Mapendekezo haya yamezingatia: malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Miaka 15 (2011/12 – 2025/26); taarifa ya awali ya maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21); Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, wakati akizindua Bunge la 11 yenye msisitizo wa ujenzi wa uchumi wa viwanda; na Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa mwaka 2015. Pia, yamezingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; makubaliano ya kikanda na Kimataifa ikiwemo: Dira ya Afrika 2063, Mpango kazi wa Kuharakisha Maendeleo ya Viwanda Afrika (2008); Sera ya Viwanda ya Afrika Mashariki pamoja na mkakati wa utekelezaji wake; Mwelekeo wa viwanda wa SADC (2013 – 2018) na Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda ya SADC (2015 – 2063).

## TATHMINI YA MWENENDO WA UCHUMI NA USTAWI WA JAMII

### (a) Mwenendo wa Uchumi

4. **Mheshimiwa Spika, Pato halisi la Taifa** lilikua kwa kiwango cha asilimia 7.0 mwaka 2014 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.3 mwaka 2013. Licha ya kupungua kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa, Tanzania imeendelea kuwa na kiwango cha juu cha ukuaji kwa nchi za Afrika Mashariki kwa mwaka 2013 na 2014. Ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika Mashariki mwaka 2014 ni kama ifuatavyo:- Rwanda (asilimia 7.0), Kenya (asilimia 5.3), Uganda (asilimia 4.9) na Burundi (asilimia 4.7).

5. **Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei** umeendelea kubaki katika kiwango cha tarakimu moja, ambapo uliongezeka kutoka

asilimia 4.0 Januari 2015 hadi asilimia 6.8 Desemba 2015; **viwango vya riba** vinaonesha kuendelea kuimarika kwa mazingira ya kupata mikopo na uwekezaji nchini ambapo tofauti kati ya riba za amana za mwaka mmoja na riba za mikopo ya mwaka mmoja iliendelea kupungua kutoka asilimia 3.43 Januari 2015 hadi asilimia 3.22 Oktoba 2015; na **thamani ya mauzo nje** ya bidhaa na huduma iliongezeka kutoka dola za Kimarekani milioni 8,610.0 Oktoba 2014 hadi Dola milioni 9,406.1 Oktoba 2015 sawa na ongezeko la asilimia 9.2. Aidha, **thamani ya Shilingi** ya Tanzania dhidi ya dola ya Kimarekani iliendelea kupungua kutoka wastani wa shilingi 1,745.6 Januari 2015 hadi shilingi 2,177.1 Oktoba 2015.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa**

**6. Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi ya Matokeo Makubwa Sasa ni pamoja na: ukarabati wa maghala 30 na ujenzi wa skimu 19 zenye jumla ya hekta 9,709 na hivyo kuwanufaisha wananchi 69,681; kukamilika kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa na maabara katika shule 167 sawa na asilimia 63.25; kuongezeka kwa ufaulu wa shule za msingi na sekondari kutoka asilimia 31 na 43 mwaka 2012 hadi asilimia 57 na 70 mwaka 2014 kwa mtiririko huo; kuunganisha umeme kwa wateja wapya 8,078 kupitia mradi wa usambazaji wa umeme vijijini awamu ya pili ambapo hadi Juni 2015, wateja waliounganishiwa umeme chini ya miradi ya REA na TANESCO wamefikia 241,401; kupungua kwa muda wa meli kukaa bandarini kwa ajili ya kupakia na kupakua mizigo kutoka siku 7.0 hadi 2.9; uchukuzi wa mizigo kwa njia ya reli umeongezeka kwa asilimia 42 kwa mwezi; kukamilika kwa ujenzi wa miradi ya maji 975 yenye

jumla ya vituo 24,129 vya kuchotea maji katika halmashauri 148 ambavyo vimenufaisha wananchi milioni 5.75; na kuanzishwa Jumuiya za Watumia Maji 1,802 ambapo Jumuiya 875 zimesajiliwa na kutoa huduma za maji vijijini kwa ufanisi.

**Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati**

**Miundombinu**

**7. Mheshimiwa Spika,** hatua iliyofikiwa Katika **reli** ni kukamilika kwa ukarabati wa mgodi wa kokoto wa Tura - Tabora na mtambo wa kuzalisha kokoto wa Kongolo – Mbeya kwa ajili ya matumizi ya njia za reli; kwa upande wa **barabara** ni kukamilika kwa ujenzi wa km 542.6 za barabara kuu ikilinganishwa na lengo la km 560.3 kwa kiwango cha lami; kukamilika kwa ukarabati wa km 102.09 za barabara kuu chini ya lengo la km 131.5 kwa kiwango cha lami; kukamilika asilimia 100 kwa ujenzi wa **bomba la gesi** kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam (km 542); kukamilika kwa ujenzi wa mitambo ya kuchakata gesi katika maeneo ya Madimba na Songosongo; kukamilika kwa vituo vya kupokelea gesi vya Somanga – Fungu na Kinyerezi; kukamilika kwa ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa Kinyerezi I; kukamilika kwa asilimia 90 ya ujenzi wa gati la **bandari ya Itungi** (Ziwa Nyasa); kukamilika kwa **Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano** (km 7,560) na kusambazwa katika mikoa 24 Tanzania Bara na kuendelea na kazi ya kuunganisha Zanzibar katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, pia kuunganisha nchi jirani za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia na Malawi; na kuboresha upatikanaji wa **huduma za maji** safi vijijini kufikia wananchi 21,783,062 sawa na asilimia 68.8.

**8. Mheshimiwa Spika,** maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo ya kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu, utalii na maeneo mengine muhimu kwa ukuaji

wa uchumi yamo katika **ukurasa wa 9 hadi 12** wa hotuba ya kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango. Aidha, ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango umeelezwa katika **Ukurasa wa 13**.

**CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI**

**9. Mheshimiwa Spika,** changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mpango pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali kukabiliana na changamoto hizo zimeelezwa katika **ukurasa wa 13 hadi 15** wa hotuba ya kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango.

**MAENEO YA VIPAUMBELE 2016/17**

**10. Mheshimiwa Spika,** baada ya kuzingatia maoni ya wadau pamoja na taarifa mbalimbali kama nilivyoainisha hapo awali, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 utakuwa na vipaumbele vifuatavyo:-

**Viwanda**

**11. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, maeneo ya vipaumbele ni: viwanda ambavyo sehemu kubwa ya malighafi yake inapatikana nchini, hususan kwenye sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, madini na maliasili nyingine; viwanda vya kuzalisha bidhaa ambazo zinatumiwa na watu wengi nchini, kama vile nguo, viatu na mafuta ya kupikia; na viwanda vinavyotumia teknolojia ya kati na kuajiri watu wengi.

**Miradi Mikubwa ya Kielelezo**

**12. Mheshimiwa Spika,** Miradi Mikubwa ya Kielelezo (flagship projects) ili kuchochea ukuaji wa uchumi. Baadhi ya miradi hiyo ni: (i) uendelezaji wa maeneo maalum ya uwekezaji (SEZ) ya

Bagamoyo, Mtwara, Kigoma na Kurasini; (ii) mji wa kilimo Mkulazi; (iii) kiwanda cha chuma cha Liganga na makaa ya mawe Mchuchuma; (iv) ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*; (v) kujenga msingi wa viwanda vya kuzalisha mitambo, nyenzo na malighafi za uzalishaji; (vi) kuimarisha huduma za usafiri wa abiria na mizigo katika maziwa makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa) ikiwa ni pamoja na ununuzi wa meli mpya, na kuimarisha Shirika la Ndege la Tanzania ikiwa ni pamoja na ununuzi wa ndege mpya; (vii) kuanza maandalizi yatakayowezesha mradi wa ujenzi wa mtambo wa kusindika gesi kimiminika (Liquified Natural Gas- LNG plant) Lindi; na (viii) kusomesha vijana wengi, hususan, katika fani zitakazohitajika zaidi za mafuta na gesi, uhandisi, kemikali, tiba na afya.

**Maeneo Wezeshi kwa Maendeleo ya Viwanda**

**13. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, maeneo wezeshi kwa maendeleo ya viwanda ni pamoja na: miundombinu ya nishati, reli, barabara, viwanja vya ndege, bandari, maji (kwa mahitaji ya viwanda) na mkongo wa Taifa wa mawasiliano. Aidha, itajumuisha kilimo (uzalishaji wa mazao, mifugo na uvuvi) kwa kuwa ni nguzo ya msingi katika kuhakikisha upatikanaji wa chakula na malighafi za uzalishaji viwandani. Katika eneo hili, msisitizo utawekwa katika miradi iliyoanza kutekelezwa katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/12 – 2015/16.

**Kufungamanisha Maendeleo ya Viwanda na Maendeleo ya Watu**

**14. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Serikali itaweka msisitizo mkubwa katika **kufungamanisha maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu**. Maeneo mahsusi yanayopendekezwa kutekelezwa ni pamoja na: kuhakikisha usalama wa chakula; afya ikiwemo kuimarisha mfumo wa

upatikanaji wa dawa kwa wananchi; kuimarisha elimu ikiwa ni pamoja na kutoa elimu msingi bila malipo, kuimarisha ubora wa elimu kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa walimu walio kazini, kuongeza matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji, kuandaa mfumo endelevu wa ugharamiaji, na kuimarisha mifumo ya ithibati na udhibiti; usimamizi na upatikanaji wa maji safi na huduma za majitaka, nishati ya uhakika, upatikanaji wa ajira, hifadhi ya jamii, usawa wa jinsia na watu wenye ulemavu, utawala bora, mipango miji na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**Maeneo Mengine**

**15. Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 yamebainisha maeneo mengine muhimu kwa ukuaji wa uchumi na ustawi wa Taifa. Maeneo hayo ni pamoja na: utalii, misitu na wanyamapori; madini; hali ya hewa; ushirikiano wa kikanda na kimataifa; na utawala bora. Katika eneo hili msisitizo utawekwa katika kukamilisha miradi ambayo utekelezaji wake ulianza katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16).

**UGHARAMIAJI WA MPANGO**

**16. Mheshimiwa Spika,** Sekta binafsi itakuwa mtekelezaji mkuu wa Mpango huu. Serikali itakuwa na wajibu wa kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi ichangie kikamilifu katika utekelezaji wa Mpango. Aidha, katika bajeti ya maendeleo ya mwaka 2016/17, Serikali inakusudia kutenga kiasi cha shilingi bilioni 6,182.2 ili kutekeleza miradi ya maendeleo, ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni 4,810.1 sawa na asilimia 77.8 ya bajeti ya fedha za maendeleo. Vile vile, Serikali itawekeza mitaji katika benki za Uwekezaji Rasilimali (TIB) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB)

ili kuvutia fedha za mikopo ya masharti nafuu kutoka taasisi za fedha za ndani na nje kugharamia miradi ya maendeleo.

**17. Mheshimiwa Spika,** Maelezo kuhusu ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa yanapatikana katika kitabu cha hotuba **ukurasa wa 19 na 20**. Aidha, maelezo kuhusu vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na hatua za kukabiliana navyo yapo katika **ukurasa wa 21 na 22** wa hotuba ya kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango.

## USHIRIKISHWAJI WA WADAU

**18. Mheshimiwa Spika**, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 yamezingatia maoni ya Wizara, Idara, na Taasisi za Serikali na Sekta binafsi. Masuala makuu ya maoni ya wadau yaliyojitokeza na kujadiliwa ni pamoja na: umuhimu wa kuandaa maeneo ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda na kuendeleza viwanda vilivyopo; upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na kupunguza utegemezi kutoka nje; na kuboresha miundombinu (maji, umeme na barabara) ili kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika viwanda nchini. Maoni na ushauri huo utazingatiwa wakati wa kuandaa Mpango wenyewe wa mwaka 2016/17.

## MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2016/17

**19. Mheshimiwa Spika,** naomba sasa nielezee kwa kifupi kuhusu Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2016/17.

**20. Mheshimiwa Spika,** Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2016/17 unawaelekeza wadau maeneo ya kuzingatia wakati wa uandaaji wa mipango na

bajeti. Aidha, Mwongozo unaonesha mwenendo wa viashiria muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ikijumuisha mapitio ya taarifa za utekelezaji wa mipango na miradi mikubwa ya kitaifa, malengo na maeneo ya vipaumbele katika kipindi cha muda wa kati, ukomo wa bajeti ya mwaka 2016/17; na mfumo wa utoaji taarifa za utekelezaji.

**21. Mheshimiwa Spika**, maelekezo ya msingi ya kuzingatiwa yametolewa katika maeneo makuu manne ambayo ni: utekelezaji wa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015; ukusanyaji wa mapato; usimamizi na udhibiti wa matumizi na ongezeko la madeni ya serikali. Aidha, Mwongozo umeainisha maeneo ya vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2016/17 ambao unalenga kujenga uchumi wa viwanda. Pamoja na vipaumbele hivyo, Mwongozo unaelekeza kutekeleza miradi na shughuli muhimu ambazo utekelezaji wake unaendelea. Vile vile, Mwongozo unatoa mapendekezo ya mfumo wa mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2016/17, ambapo jumla ya Shilingi bilioni 22,991.4 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho, sawa na ongezeko la asilimia 2.2 ya makisio ya bajeti ya mwaka 2015/16. Ongezeko hilo litatokana na kuimarika kwa jitihada za ukusanyaji wa mapato ya ndani na kutarajiwa kupungua kwa fedha za misaada na mikopo nafuu.

## UTEKELEZAJI WA BAJETI YA NUSU MWAKA YA 2015/16

**22. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/16, Serikali ilipanga kukusanya na kutumia kiasi cha shilingi bilioni 22,495.5. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2015, mapato yote ya Serikali yalikuwa jumla ya shilingi bilioni 10,237.7 ikiwa ni sawa na asilimia 88.8 ya makadirio ya nusu mwaka. Aidha, hadi kufikia Desemba 2015, Serikali imetoa mgao wa matumizi wenye thamani

ya shilingi bilioni 10,312.4 sawa na asilimia 89 ya lengo la shilingi bilioni 11,531.1 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi kilichotolewa, shilingi bilioni 8,181.5 zilikuwa ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 2,130.9 ni matumizi ya maendeleo. Mafanikio, changamoto, pamoja hatua za kukabiliana na changamoto hizo umeelezewa katika **ukurasa wa 10 na 12** wa hotuba ya kuwasilisha Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17. Aidha, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2014/15, mafanikio, changamoto, pamoja hatua za kukabiliana na changamoto hizo umeelezewa katika **ukurasa wa 6 na 9** wa hotuba ya kuwasilisha Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17.

## MAMBO MUHIMU KATIKA KUANDAA MWONGOZO WA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA 2016/17

**23. Mheshimiwa Spika,** katika uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2016/17 Serikali inatarajia kusimamia mambo muhimu kama ifuatavyo:

### a) Shabaha za Uchumi Jumla

**24. Mheshimiwa Spika,** Shabaha na malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha 2016/17 – 2020/21 ni kama ifuatavyo:-

(i) Pato Halisi la Taifa kukua kwa asilimia 7.0 mwaka 2015, asilimia 7.2 mwaka 2016, na kuendelea kuongezeka hadi wastani wa asilimia 8 katika kipindi cha muda wa kati kwa kutumia takwimu zilizorekebishwa za mwaka wa kizio wa 2007;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja kufikia asilimia 6.0 Juni 2016 na kubaki kati ya asilimia 5 na asilimia 8 katika kipindi cha muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri kufikia asilimia 14.8 ya Pato la Taifa mwaka 2016/17, asilimia 15.1 mwaka 2017/18, na asilimia 16.3 mwaka 2019/20;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.2 ya Pato la Taifa mwaka 2016/17, asilimia 13.5 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18 na kufikia asilimia 14.4 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2019/20;

(v) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kupungua kutoka asilimia 23.9 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16 hadi asilimia 21.5 mwaka 2016/17 kufuatia kukamilika kwa uchaguzi mkuu;

(vi) Kupunguza nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kutoka asilimia 4.2 mwaka 2015/16 na kuendelea kupungua hadi chini ya asilimia 3.0 katika kipindi cha muda wa kati;

(vii) Kasi ya ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) kuwa asilimia 16.0 Juni 2016 na kupungua kufikia asilimia 15.6 Juni 2017 na kubakia katika kiwango cha wastani wa zaidi ya asilimia 14.0 katika kipindi cha muda wa kati sambamba na lengo la kupunguza mfumuko wa bei;

(viii) Nakisi katika urari wa malipo ya kawaida kuwa asilimia 9.4 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16 na kuendelea kupungua hadi chini ya wastani wa asilimia 8 katika kipindi cha muda wa kati; na

(ix) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

**b) Misingi ya Mpango na Bajeti**

**25. Mheshimiwa Spika**, Misingi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika kipindi cha mwaka 2016/17 ni pamoja na:-

(i) Amani, usalama, na utulivu wa ndani na nchi jirani vitaendelea kuimarishwa na kudumishwa;

(ii) Viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kama vile Pato la Taifa, biashara ya nje, ujazi wa fedha, mapato na

matumizi na viashiria vya huduma za jamii vitaendelea kuimarika;

(iii) Sera za fedha zitaendelea kuimarishwa ili ziendane na sera za bajeti zitakazosaidia kupunguza mfumuko wa bei na tofauti kati ya riba za amana na za mikopo;

(iv) Kuendelea kuimarika na kutengemaa kwa uchumi wa dunia;

(v) Bei za mafuta katika soko la dunia zitaendelea kuwa nzuri; na

(vi) Hali nzuri ya hewa nchini na katika nchi jirani.

**c) Mfumo wa Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2016/17**

**26. Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia sera za uchumi pamoja na misingi na sera za bajeti kwa mwaka 2016/17, Sura ya Bajeti inaonesha kuwa jumla ya Shilingi bilioni 22,991.5 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho. Jumla ya mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yanatarajiwa kuongezeka kufikia Shilingi bilioni 15,801.2, sawa na asilimia 68.7 ya mahitaji yote ikilinganishwa na asilimia 62.2 mwaka 2015/16.

**27. Mheshimiwa Spika,** kati ya mapato hayo, Serikali inalenga kukusanya mapato ya kodi ya jumla ya Shilingi bilioni 14,106.6 sawa na ongezeko la asilimia 14.1 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2015/16. Aidha, mapato yasiyo ya kodi na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri ni Shilingi bilioni 1,110.2 na Shilingi bilioni 584.4 kwa mtiririko huo. Serikali inategemea kukopa kiasi cha Shilingi bilioni 1,782.3 kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara. Aidha, mikopo ya ndani inakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 3,300.5 zikijumuisha Shilingi bilioni 2,766.1 kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva.Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia Shilingi bilioni 2,107.4 ikiwa

ni misaada na mikopo, sawa na asilimia 9.3 pungufu ya makadirio ya mwaka 2015/16.

**Vyanzo vya Mapato ya Ndani Kwa Mwaka 2016/17**

**28. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Serikali inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 14,139.0 (pamoja na TVCs) kutoka kwenye vyanzo vya kodi, sawa na asilimia 13.2 ya Pato la Taifa. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 15 ikilinganishwa na matarajio ya kukusanya jumla ya shilingi bilioni 12,307.9 kwa mwaka 2015/16.

**29. Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa vyanzo vya mapato ya ndani (Jedwali limeambatishwa) hadi sasa ni pamoja na vifuatavyo:

i. Kodi za moja kwa moja (Direct Taxes). Chanzo hiki kinajumuisha kodi ya mapato ya watumishi (PAYE), kodi ya mapato ya Watu Binafsi (Individuals), Tozo ya Kuendeleza Ujuzi (Business and Skills Developement Levy) Kodi ya Makampuni (Corporation Tax), kodi za zuio (Witholding Taxes) pamoja na kodi nyinginezo ikiwa ni pamoja na kodi kutokana na michezo ya kubahatisha. Jumla ya mapato kutoka eneo hili ni shilingi bilioni 5,298.7;

ii. Kodi za ndani zisizo za moja kwa moja (Indirect Taxes – Domestic). Chanzo hiki kinajumuisha kodi za ushuru wa bidhaa za ndani kama vile vinywaji mbalimbali, sigara na muda wa matumizi kwa simu za viganjani; Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa bidhaa na huduma za ndani. Jumla ya mapato katika eneo hili ni shilingi bilioni 3,920.9; na

iii. Kodi zitokanazo na Biashara za Kimataifa (International Trade Taxes). Chanzo hiki kinajumuisha kodi ya Ushuru wa Forodha, kodi mbalimbali zinazotozwa kwenye bidhaa za mafuta kama vile Fuel levy, ushuru wa bidhaa kwenye

mafuta (Excise duty on petroleum), Petroleum Fee-REA, kodi ya ongezeko la thamani (VAT on imports), ushuru wa bidhaa pamoja na ushuru wa mifuko ya maendeleo ya Reli na Maji. Katika eneo hili Serikali inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 5,812.9.

**30. Mheshimiwa Spika,** Aidha, jumla ya marejesho ya kodi kwa mwaka 2016/17 yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 925.9 na hivyo kufanya mapato halisi (net) kufikia shilingi bilioni 14,106.6. Vocha za Hazina (Treasury Vouchers – TVCs) zinakadiriwa kufikia shilingi bilioni 32.4 na hivyo, mapato yote pamoja na Vocha za Hazina kufikia shilingi bilioni 14,139.0.

**Matumizi**

**31. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi, katika mwaka 2016/17 Serikali inapanga kutumia jumla ya Shilingi bilioni 22,991.5 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 16,809.2 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha Shilingi bilioni 6,651.5 kwa ajili ya mishahara. Aidha, matumizi ya maendeleo yatakuwa Shilingi bilioni 6,182.2 ambapo kiasi cha Shilingi 4,810.1 ni fedha za ndani sawa na asilimia 77.8 ya fedha za maendeleo.

**32. Mheshimiwa Spika,** sehemu kubwa ya fedha za bajeti ya maendeleo zitatumika kugharamia miradi ya huduma za kijamii, na kiasi kidogo kitatumika kama mtaji (equity) wa kuwekeza kwenye miradi inayoweza kutupatia mapato (revenue generating projects) ambapo wakopeshaji wataongeza mtaji huo na kusimamia utekelezaji wa mradi husika. Aidha utaratibu wa PPP utatumika kuipunguzia serikali gharama za utekeleaji wa miradi ya maendeleo.

**d) Maelekezo ya Mwongozo**

**33. Mheshimiwa Spika,** Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17 umeainisha mambo muhimu yanayotakiwa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli ambayo ni: Utayarishaji wa bajeti kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015; ukusanyaji wa mapato; usimamizi wa matumizi ya Serikali na hatua za kupunguza gharama; na kulipa na kuzuia ongezeko la madeni ya Serikali. Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuzingatia yafuatayo katika maeneo hayo:

**Utekelezaji wa Sheria ya Bajeti**

**34. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 ulianza tarehe 1 Julai, 2015. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaagizwa kuzingatia Sheria hii na Kanuni zake za mwaka 2015 katika maandalizi na utekelezaji wa Mipango na Bajeti za Mafungu yao. Aidha, Sheria hii inaelekeza maafisa masuuli kuunda Kamati za Bajeti na kuwezesha kufanyika kwa mikutano ya maandalizi ya Mpango na Bajeti ya fungu husika. Majukumu ya kamati za bajeti yameainishwa katika kifungu cha 17(3) cha Kanuni za Bajeti za mwaka 2015. Kamati za bajeti zinawajibika kutimiza majukumu hayo, pamoja na kuzingatia nyaraka za Msajili wa Hazina na nyaraka nyingine za Serikali

**Ukusanyaji wa mapato ya Serikali**

**35. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Mapato yote yatakusanywa na Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo basi, Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara za Serikali, Wakala, Taasisi, Sekretarieti za Mikoa, na

Mamlaka za Serikali za Mitaa isipokuwa yale yanayokusanywa kwa mujibu wa sheria ya fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Namba 9 ya mwaka 1982 inayoruhusu Mamlaka hizo kukusanya mapato kwenye maeneo yao na kuyatumia, watatakiwa kuwasilisha mapato yote yatakayokusanywa yawasilishwe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na yatagawiwa kulingana na bajeti za mafungu zitakazoidhinishwa;

(ii) Utaratibu wa 'Retention' uliokuwa ukitumika awali umefutwa. Hivyo, mapato yote yatakusanywa na kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kila fungu litapewa fedha kulingana na bajeti yake;

(iii) Majengo ambayo hayajafanyiwa uthamini yatozwe kodi kwa makundi. Zoezi hili lifanyike katika Majiji, Manispaa, Halmashauri za Miji, Makao Makuu ya Halmashauri za Wilaya na Mamlaka za Miji Midogo kwa kipindi cha mpito wakati zoezi la uthamini wa majengo hayo likikamilishwa;

(iv) Kuainisha vyanzo vyote vya mapato kama moja ya mkakati wa kuboresha ukusanyaji wa mapato;

(v) Kuboresha mazingira ya urasimishaji wa biashara ili kupanua wigo wa kodi;

(vi) Kusimamia ipasavyo upatikanaji na matumizi sahihi ya mashine za kielektroniki (EFD);

(vii) Kufanya mapitio ya mikataba yote iliyopewa misamaha ya kodi ili kutathmini faida zake na kujipanga upya;

(viii) Kuhakikisha taasisi zote umma zinatumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa kodi, ada, ushuru na tozo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

(ix) Kuingia mikataba na wazabuni, makandarasi na watoa huduma wanaotumia mashine za kielektroniki; na

(x) Kupitia upya viwango vya ada, ushuru na tozo ili kuzirekebisha ziendane na viwango vya soko katika kutoa huduma za umma.

**Usimamizi wa Matumizi na Hatua za Kupunguza Gharama**

**36. Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia na kudhibiti matumizi ya Serikali, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kuhakikisha mikutano yote ikiwa ni pamoja na mikutano ya bodi, mafunzo na semina inatumia kumbi za Serikali na Taasisi za Umma;

(ii) Kutoa kipaumbele kwa Taasisi za Umma katika kununua huduma kama vile bima, usafirishaji wa barua, mizigo na vifurushi (courier), matangazo na usafiri;

(iii) Kuhakikisha Mashirika ya umma yaliyoundwa kwa lengo la kujiendesha kibiashara, yanajiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku ya Serikali. Mashirika hayo ni pamoja na TANESCO, TAZARA, TRL, ATCL, RAHCO, TEMESA, Wakala wa Vipimo (WMA), Bodi ya Mazao Mchanganyiko;

(iv) Kudhibiti matumizi ya umeme, simu na maji ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara;

(v) Kudhibiti ulipaji wa mishahara kwa watumishi wanaostahili na waliopo katika vituo vya kazi. Aidha Wizara ya Fedha na Mipango itafanya sensa ya watumishi wote ili kuondokana na watumishi wanaolipwa bila kustahili;

(vi) Kuendelea kufanya ununuzi wa bidhaa na huduma kwa pamoja/wingi (in bulk) kutoka kwa wazalishaji au watengenezaji ili kupata nafuu ya bei. Hivyo, matumizi ya Wakala hayaruhusiwi;

(vii) Kuendelea na ununuzi wa pamoja wa magari kupitia GPSA baada ya Maafisa Masuuli kupata vibali vya ununuzi

kutoka kwa Waziri Mkuu;

(viii) Kupunguza gharama katika maeneo mbalimbali ikiwemo matengenezo ya magari, mafuta ya magari, sherehe, matamasha, na safari za nje ya nchi;

(ix) Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali katika ngazi zote;

(x) Kudhibiti matumizi ya taasisi za Serikali yasiyo na tija na kufanya tathmini ya gharama za uendeshaji ili kuchukua hatua stahiki kwa maendeleo ya nchi; na

(xi) Kusimamia kikamilifu Sheria ya Ununuzi wa Umma ili kuhakikisha kwamba mianya yote ya fedha za umma inayotokana na usimamizi hafifu inazibwa.

**Kulipa na Kuzuia Ongezeko la Madeni ya Serikali**

**37. Mheshimiwa Spika,** katika kudhibiti ulimbikizaji wa madeni, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia kifungu Na. 52(1) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Waraka wa Hazina Na. 4 wa tarehe 31 Desemba, 2014 kwa kufanya yafuatayo:

(i) Kulipa madeni yale tu yaliyohakikiwa na kuingizwa kwenye hesabu za Serikali (Financial statement);

(ii) Kuwasilisha kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali taarifa ya madeni iliyokaguliwa na Mkaguzi wa ndani wa fungu na kuidhinishwa na Afisa Masuuli wa fungu husika;

(iii) Kuzingatia maagizo na maelekezo mbalimbali yaliyokwisha kutolewa na Serikali siku za nyuma kuhusu ununuzi wa bidhaa na huduma mfano ununuzi wa samani, kuhamisha watumishi, ununuzi wa magari, ulipaji na uzuiaji wa malimbikizo ya madeni;

(iv) Kutumia LPO zinazotolewa kwenye mfumo wa IFMS katika kupata huduma; na

(v) Kudhibiti uingiaji wa mikataba ya miradi inayotekelezwa kwa zaidi ya mwaka mmoja kwa kuzingatia Kifungu Na.

52 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015.

**HITIMISHO**

**38. Mheshimiwa Spika,** Serikali itahakikisha kuwa inaimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuelekeza matumizi kwenye maeneo yenye tija kwa manufaa ya watanzania wote. Ni matumaini yangu kuwa wadau wote wanaohusika katika uandaaji na utekelezaji wa mwongozo huu watazingatia maelekezo yaliyopo ili kuhakikisha malengo na matarajio ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2016/17 yanatimia.

**39. Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe hotuba yangu kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii na kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/17 vinapatikana katika tovuti za Wizara ya Fedha na Mipango www.mof.go.tz na www.mipango. go.tz.

**40. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lijadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2016/17 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2016/17. Serikali itazingatia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na kuyafanyia kazi ipasavyo wakati wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2016/17.

**41. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.